

9. Yesu anasema...Pokea busu zitakazokubadilisha zinazotoka Mungu wako na uponywe (English Title - Receive the transforming Kisses from God)

Neno Kinabii

Oktoba 31st, 2014 - Neno kutoka Yesu kwa Dada Clare (kutafsiriwa na Louis)

Yesu angependa kukupatia busu, na kucheza densi na wewe, na kuchunguza na wewe uzuri wa Mbinguni na yeye. Yesu angependa kupewa busu nawe. Kubadilishana kwa moyo kwa usafi na Yesu, ndicho kitu ambacho Anachotamani sana kutoka Bibi Harusi wake. Yesu atakubusu kwa roho yako, kwasababu wewe ni dhabahu kwake, Bibi wake wa harusi, na hapatakuwa na kitu chochote kibaya kuihusu.

"Hizi busu kutoka Kwangu zitakubadilisha kutoka kuwa chombo cha matope hadi ukuwe chombo cha dhahabu ya upendo wa Mungu, ukiloweshwa kwa upendo Wangu. Nitaponya vidonda, kovu, zile nafasi tupu zilizokuwa zimejazwa na furaha kitambo walakini zilisalitiwa na kupotea milele. Zile pahali zinazouchungu undani wa roho zenu, ambapo nitakapo mwaga mafuta ya upendo ndani na kuwapatia ukamili na kufura kwa roho zenu maji ya maisha yale ambayo kila roho utakaye patana naye anatamani kukunywa kwingi. Walakini ujue haitawezekana ukinipekua na kuamini uwongo wa shetani anayejaribu kuvunja uhusiano Yangu na wewe.

"Unao marafiki waliohuzunika kwa ajili ya talaka? Uchungu wanaohisi utaweza kuponywa kamili na upendo wangu, ila tu kama ungependa kunitafuta mpaka ungenipata, ili utaweza kuingia pahali pangu pa kupumzika na ukubali mafuta ya furaha iweze kuosha kwa undani vidonda vyako vyote.

"Unahuzunika kwa ajili ya kifo ya mpwendwa wako ambaye aliaga dunia kwa ajili ya ugonjwa wa kansa? Hii huzuni na uchungu inaweza kuponywa, na wewe kupata kuelewa kwa undani, na pia kujazwa na upendo ili uweze kumwaga hii mafuta yanayotoka kwangu Yesu kwa roho zingine zilizohuzunika."

"Umechanganyikiwa na kujazwa na huzuni kuhusu vitendo usivyoweza kukamilisha ama vile ulivyoshindwa duniani? Ndoto zako kutokamilika? Alafu pia unapata kwamba siku zako za mbele hazina nia?"

"Keti na mimi. Kubali upendo wangu uweze kurejesha hayo matumaini yako. Kubali niweze kuiingia hizi sehemu za giza na upweke, nikizijaza na upendo wangu na utaweza kuepuka giza na upweke unaohisi. Nitakuongoza maisha yako nikikujaza na maji ya uzima, nikikuonyesha mwisho wa ndoto zako mahali ambapo zawadi, talanta na ndoto zako zote zitakazokamilika kwa ajili ya nguvu za neema Yangu ambayo itakayofanya kazi ndani yako."

"Nakwambia ukweli, hamna kidonda ya undani sana, hakuna ndoto nisyoweza kukamilisha, hakuna maisha nisyoweza kuokoa. Nitakuletea uzima na ukamili wa maisha yako, ila tu ukifanya vile vitendo ulivyoumbwa kufanya kwa jina langu Yesu Kristu Bwana wetu."

"Nasema tena, zaidi ya ndoto zako kupindukia"